

Korosho changa huanza kukauka



*Korosho changa huwa nyeusi
mithili ya rami na hukauka
kabisa*



Korosho changa huweza kudondoka chini

• **Tumia mbegu bora**

- ✓ Tumia mbegu bora za korosho zinazopatikana kwenye Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Maendeleo Naliendele na vituo vyake vya uendelezaji wa zao hilo.


- ✓ Hakikisha vikonyo vya kubebesha ni safi na salama dhidi ya ugonjwa.

• **Viuatilifu.**

Tumia viuatilifu vyenye viambata sumu aina ya ‘*Trifloxistrobin*’ au ‘*Picoxystrobin*’.



Pulizia viuatilifu kudhibiti Blaiti



UGONJWA WA BLAITI YA MIKOROSHO



Kimetayarishwa na:

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509,
MTWARA
Email : cdnaliendele@tari.go.tz

UGONJWA WA BLAITI YA MIKOROSHO

Utangulizi.

Blaiti ni moja ya magonjwa makubwa yanayoathiri uzalishaji wa korosho Ugonjwa huu unasababishwa na vimelea aina ya uyoga. Nchini Tanzania ulianza kuonekana mwaka 2004 na kwa sasa umeenea katika maeneo mengi yanayolima korosho.

Mashambulizi na Dalili za Ugonjwa



Majani ya korosho yaliyo shambuliwa na ugonjwa wa blaiti na kukauka

- Blaiti hushambulia sehemu zote teke kama vile majani, mabibo na korosho changa
- Majani hubabuka na kuwa na mabaka makubwa, hatimaye hudondoka chini.
- Mabaka meusi huoneka getu na kwenye mabibo



Korosho changa huanza kuwa na mabaka meusi

Hali ya hewa inayostawisha Ugonjwa

- Ugonjwa huu hushamiri sana baada manyunyu au mvua kunyesha.
- Husambazwa na mvua na upepo.



Mabibo machanga hugeuka meusi

Njia za kudhibiti

- **Kusa fisha Mashamba**
 - ✓ Kusanya na choma moto majani na tegu zilizo sham bu liwa au
 - ✓ Chimba mashimo na ku fukia majani m achanga ya liyo sham bu liwa.